MWONGOZO WA
UTAWALA BORA

policy forum

MWONGOZO WA UTAWALA BORA

policy forum

Kimetayarishwa na:
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Kikundi Kazi cha Serikali za Mitaa cha Policy Forum

Mchora katuni: Nathan Mpangala

Kimechapishwa na Policy Forum
Toleo la kwanza - Septemba, 2013

ISBN: 978-9987-708-09-3

Kimesanifiwa na kupigwa chapa na:
Tanzania Printers Limited
S.L.P. 451, Dar es Salaam, Tanzania

YALIYOMO

DIBAJI iv
SURA YA 1 1
1.0 UTAWALA BORA 1
1.2 Faida za Utawala Bora 2
SURA YA 2 3
2.0 MISINGI YA UTAWALA BORA 3
2.1 Uwazi 3
2.2 Uwajibikaji 3
2.3 Utawala wa Sheria 4
2.4 Ushirikishwaji 4
2.5 Usawa 5
2.6 Ufanisi na Tija. 5
2.7 Mwitikio 5
2.8 Maridhiano 6
2.9 Uadilifu 6
SURA YA 3 7
3.0 NGUZO ZA UTAWALA BORA 7
3.1 Katiba ya Kidemokrasia 8
3.2 Ulinzi, Ukuzaji na Uzingatiaji wa Haki za Binadamu 8
3.3 Mgawanyo wa Madaraka 8
3.4 Uhuru wa Mahakama 9
3.5 Uhuru wa Habari na Uhuru wa Vyombo vya Habari 9
SURA YA 4 10
4.0 HAKI ZA BINADAMU 10
4.1 Vyanzo vya Haki za Binadamu nchini Tanzania 10
4.2 Haki za Binadamu kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Ibara ya 12 - 24) 11
4.3 Uhusiano kati ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora. . 15
SURA YA 5 17
5.0 MISINGI YA UTOAJI WA HAKI 17
5.1 Kanuni za Haki ya Asili 18
HITIMISHO 19

DIBAJI

Kijitabu hiki cha ***Mwongozo wa Utawala Bora*** ni mfululizo wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na Policy Forum ya kukuza utawala bora nchini. Vile vile, kijitabu hiki ni mchango wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na Policy Forum katika kusaidia juhudi za Serikali za kuimarisha utawala bora katika ngazi zake zote.

Lengo kuu la kijitabu hiki ni kukuza utawala bora nchini. Malengo mengine ni kuongeza uelewa wa watendaji, wananchi na viongozi kuhusu utawala bora na haki za binadamu.

Msomaji wa kijitabu hiki atajifunza maana ya utawala bora, faida za utawala bora, athari za kukosa utawala bora, misingi ya utawala bora, nguzo za utawala bora, haki za binadamu, misingi ya haki za binadamu, vyanzo vya haki za binadamu, uhusiano kati ya haki za binadamu na utawala bora na misingi ya utoaji wa haki.

Tunaamini kuwa kijitabu hiki kitasaidia katika kujenga jamii ambayo misingi ya utawala bora na haki za binadamu inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na kuhifadhiwa.

Shukrani ziwaendee maafisa wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (ambao ni Vincent Mbombo, Emmanuel Barigila na Pontian Kitorobombo) pamoja na Kikundi Kazi cha Serikali za Mitaa (LGWG) cha Policy Forum kwa kuandaa kijitabu hiki.

Fatuma I. Muya,
Mkurugenzi wa Idara ya Utawala Bora,
Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
Septemba, 2013

Hebron Mwakagenda,
Mwenyekiti wa Kikundi Kazi cha Serikali za Mitaa,
Policy Forum.
Septemba, 2013

SURA YA 1

1.0 UTAWALA BORA

Utawala ni matumizi ya mamlaka ya kisiasa, kiuchumi au vinginevyo katika kusimamia masuala ya nchi kwenye ngazi zote.

Utawala bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu usawa na unafuata utawala wa sheria.

Ili kutekeleza dhana ya utawala bora mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:

- Matumizi sahihi ya dola,
- Matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi,
- Matumizi mazuri ya madaraka yao,
- Kujua na kutambua madaraka waliyonayo na matumizi yake,
- Madaraka yanatumika kulingana na mipaka iliyowekwa na katiba na sheria.

1.2 Faida za Utawala Bora

Utawala bora unasaidia kuwa na mambo yafuatayo:

- Matumizi mazuri ya rasilimali za nchi,
- Maendeleo endelevu,
- Kupungua kwa umasikini, ujinga na maradhi,
- Kutokomea kwa rushwa,
- Huduma bora za jamii,
- Amani na utulivu,
- Kuheshimiwa kwa haki za binadamu,
- Utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa sheria na taratibu,
- Kuleta ustawi wa wananchi.

SURA YA 2

2.0 MISINGI YA UTAWALA BORA

2.1 Uwazi

Uwazi ni hali ya kuendesha shughuli za umma bila usiri na kificho ili wananchi wawe na uwezo wa kupima utendaji na uzingatiaji wa kanuni, taratibu na sheria. Uwazi unajumuisha:

- Wananchi kupata taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti za kutekeleza mipango hiyo, kwa lugha rahisi na kwa wakati;
- Wananchi kupewa taarifa za mapato na matumizi;
- Wananchi kufahamishwa huduma zinazotolewa bila malipo na huduma wanazopaswa kuchangia, na utaratibu wa kupata huduma hizo;
- Wananchi kujulishwa mahali na wakati muafaka wa kupata taarifa wanazozihitaji na wazipate bila usumbufu; na
- Kupewa sababu na uhalali wa maamuzi yaliyofikiwa na viongozi wao.

2.2 Uwajibikaji

Uwajibikaji ni hali ya kiongozi na mtendaji kuwa tayari kujibu, kubeba dhamana na kutoa maelezo kwa wananchi juu ya maamuzi au matendo aliyoyafanya katika kutekeleza dhamana aliyopewa. Kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (c) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*, 1977 Serikali (viongozi na watendaji) itawajibika kwa wananchi.

2.3 Utawala wa Sheria

Utawala wa Sheria unamaanisha mambo yafuatayo:

- Mfumo wa sheria za nchi ulio wa haki na ambao umejengwa na sheria zisizo kandamizi;
- Usawa mbele ya sheria: watu wote wawe sawa mbele ya sheria;
- Uendeshaji wa shughuli za umma pamoja na maamuzi lazima vifanyike kwa kufuata sheria za nchi; na
- Ulinzi na haki sawa mbele ya sheria.

2.4 Ushirikishwaji

Ni kuwahusisha wananchi wa jinsia zote na makundi yote katika kupanga na kufanya maamuzi ya mambo yanayowahusu. Ushirikishwaji unaweza ukawa wa moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi.

2.5 Usawa

Ni hali ya kuwapatia wananchi wote fursa sawa katika kushiriki kwenye mambo yanayohusu jamii yao. Usawa katika utendaji unahusisha mambo yafuatayo:

- Kutoa huduma bila ubaguzi au upendeleo wa aina yoyote.
- Kuendesha shughuli za umma bila ubaguzi au upendeleo.
- Kuthamini watu wote bila kujali tofauti zao.
- Kutambua makundi yote katika jamii na kutoa fursa sawa kwa makundi yote katika kuboresha hali zao.
- Kumfanya kila mwanajamii kujiona kuwa yeye ni sehemu ya jamii na pia ana maslahi kwenye jamii yake.

2.6 Ufanisi na Tija.

Ufanisi na tija ni hali ya utendaji inayozalisha matokeo yanayokidhi malengo na matarajio ya watu na kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali. Ufanisi na Tija unajumuisha mambo yafuatayo:

- Utendaji wenye matokeo yanayokidhi malengo na matarajio ya watu wote.
- Kutumia rasilimali kwa uangalifu na umakini (Matumizi bora ya rasilimali).
- Utumiaji endelevu wa rasilimali.
- Utunzaji wa mazingira.
- Utoaji wa uhakika wa huduma za jamii.

2.7 Mwitikio

Ni hali ya kutoa huduma kwa jamii kwa wakati na kwa kiwango kinachokidhi matarajio ya watu. Mwitikio unajumuisha mambo yafuatayo:

- Kujali na kusikiliza matatizo ya watu.
- Kutoa huduma kwa haraka na kwa kiwango bora.
- Kukidhi matarajio ya watu.

2.8 Maridhiano

Utawala bora unahimiza kukutanishwa kwa mawazo mbalimbali ili kupata suluhu au maamuzi ya pamoja ambayo yanazingatia matakwa ya jamii nzima.

2.9 Uadilifu

Ni hali ya kuwa mwaminifu na kuwa na mwenendo mzuri katika utendaji kazi. Uadilifu unahusisha kujali watu, kujali muda, kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, kuepuka vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kuwa mkweli, kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

SURA YA 3

3.0 NGUZO ZA UTAWALA BORA

Dhana ya Utawala Bora ina nguzo kuu sita:

- Katiba ya kidemokrasia;
- Ulinzi, ukuzaji na uzingatiaji wa haki za binadamu;
- Mgawanyo wa Madaraka;
- Uhuru wa Mahakama;
- Uhuru wa habari na
- Uhuru wa vyombo vya habari.



3.1 Katiba ya Kidemokrasia

Katiba ni waraka wa kisiasa na kisheria wenye muafaka wa kitaifa juu ya namna ya kuendesha masuala ya nchi.

Demokrasia ni mfumo wa kisiasa wa kuchagua na kubadilisha serikali kwa njia ya uchaguzi ulio huru na wa haki. Ni Ushirikishwaji wa kweli wa wananchi katika maisha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Hivyo, **Katiba ya Kidemokrasia** ni ile ambayo kuandikwa kwake kumetokana na ridhaa na mwafaka wa wananchi.

3.2 Ulinzi, Ukuzaji na Uzingatiaji wa Haki za Binadamu

Utawala bora ni ule unaolenga kuboresha na kujali maisha ya watu. Njia ya msingi ya kujali maisha ya watu ni kulinda, kukuza na kuzingatia haki za binadamu. Utawala bora unataka kuwe na mfumo wa kisheria, kiutawala na utashi wa kisiasa unaolinda, kukuza na kuzingatia haki za binadamu.

3.3 Mgawanyo wa Madaraka

Dhana ya mgawanyo wa madaraka inaeleza kuwa utawala wa dola unapaswa kugawanywa katika vyombo vitatu ambavyo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Kila chombo kina majukumu tofauti na chombo kingine.

Kwa mujibu wa dhana hii, mamlaka ya Serikali ni utendaji; mamlaka ya Bunge ni kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma; na mamlaka ya Mahakama ni kutafsiri sheria na kutoa haki. Hapa nchini, dhana hii inatajwa kwenye Ibara ya 4 ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ya mwaka 1977.

Dhana hii inazuia chombo kimoja kutawala, kuingilia na kufanya kazi za chombo kingine. Lengo la mgawanyo wa madaraka ni kuongeza ufanisi na kuleta uwajibikaji wa vyombo vya dola.

3.4 Uhuru wa Mahakama

Uhuru wa Mahakama unamaanisha kuwa kila jaji au hakimu yuko huru kuamua kesi iliyopo mbele yake kwa mujibu wa sheria na ushahidi ulioletwa mbele yake, na katika kutekeleza majukumu hayo, hapaswi kuingiliwa, kushawishiwa, au kushinikizwa na mtu au chombo chochote, ikiwemo Bunge na Serikali kama inavyoelezwa katika Ibara ya 107B ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ya mwaka 1977. Hivyo, dhana ya uhuru wa mahakama inaitaka mahakama kutekeleza majukumu yake bila woga wala upendeleo.

Uhuru wa mahakama unahifadhiwa na kulindwa katika maeneo manne ambayo ni:

i) Kuzuia kuondolewa kwa Jaji au Hakimu katika ofisi bila ya sababu za msingi na bila ya kufuata taratibu zilizowekwa hata kama kuna sababu za kumuondoa,

ii) Kuweka kinga ya kutoshtakiwa kwa Jaji au Hakimu kwa makosa yoyote, yawe ya jinai au madai kutokana na maamuzi yake ya kimahakama aliyoyafanya,

iii) Kutopunguza au kuondoa mishahara na maslahi ya Jaji au Hakimu, na

iv) Kutokuwa na vyeo kwenye vyombo vingine vya dola au kushiriki katika shughuli za vyama vya siasa.

Hata hivyo, ni vema ikafahamika kwamba uhuru wa mahakama sio kibali kwa jaji au hakimu kuamua kesi kwa namna anavyojisikia yeye au kwa matakwa yake.

3.5 Uhuru wa Habari na Uhuru wa Vyombo vya Habari

Uhuru wa habari una maana ya watu kuweza kuzungumza na kupashana habari na kuwa na haki ya kupata habari kutoka katika vyombo vya umma na hata binafsi ambavyo vinatekeleza wajibu wa umma. Hili lazima liende sawia na kuwa na vyombo vya habari vilivyo huru, kwa maana ya kuwa na uwezo wa kutafuta na kuandika habari na kuzisambaza kwa watu ndani na nje ya mipaka ya nchi bila ya kuingiliwa na bila ya sababu maalum na Serikali. Lengo ni kuwawezesha wananchi kufahamu namna viongozi wanavyoendesha nchi na hatimaye kujadili na kutoa maamuzi juu ya rasilimali za nchi yao.

SURA YA 4

4.0 HAKI ZA BINADAMU

Haki za binadamu ni stahili alizonazo kila binadamu kwa asili ya kuwa binadamu.

4.1 Vyanzo vya Haki za Binadamu nchini Tanzania

Chanzo kikuu cha haki za binadamu nchini Tanzania ni *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977*. Sambamba na Katiba, vipo vyanzo vingine vya haki za binadamu nchini, kama vile, *Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009*, *Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Namba 9 ya mwaka 2010*, *Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Ukimwi Namba 28 ya mwaka 2008*, *Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004*, *Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 (R.E. 2002)* na mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ya kimataifa na ya kikanda ambayo Tanzania imeisaini na kuiridhia.

4.2 Haki za Binadamu kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Ibara ya 12 - 24)

Haki zinazotajwa kwenye ibara za 12 hadi 24 za *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977* ni kama ifuatavyo:

S/N	HAKI ZA BINADAMU	MCHANGANUO WAKE
1	**Haki ya Usawa wa Binadamu** ***(Ibara ya 12)***	• Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.
		• Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.
2	**Usawa mbele ya Sheria** ***(Ibara ya 13)***	• Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.
		• Haki ya kutobaguliwa na sheria iwe kwa dhahiri au kwa taathira.
		• Haki ya kutobaguliwa na mtu au mamlaka yoyote.
		• Haki ya kusikilizwa
		• Haki ya mtu kutoteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha.
3	**Haki ya Kuwa Hai** ***(Ibara ya 14)***	• Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria.

4	**Haki ya Uhuru wa Mtu Binafsi** ***(Ibara ya 15)***	• Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru
		• Ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu:- a) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria; au b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.
5	**Haki ya faragha na ya usalama wa mtu** ***(Ibara ya 16)***	• Kila mtu ana haki ya kuheshimiwa.
		• Kila mtu ana haki ya kupata hifadhi ya nafsi yake, maisha yake binafsi, familia yake na unyumba wake.
		• Kila mtu ana haki ya hifadhi ya maskani ya mtu na mawasiliano yake binafsi.
6	**Uhuru wa Mtu kwenda atakako** ***(Ibara ya 17)***	• Kila raia wa Jamhuri ya Muungano ana haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
		• Kila raia ana haki ya kuishi sehemu yoyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
		• Haki ya raia kutoka nje ya nchi na kuingia nchini
		• Haki ya raia kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7	**Uhuru wa maoni** ***(Ibara ya 18)***	• Haki ya mtu kuwa na maoni na kutoa nje mawazo yake.
		• Haki ya kutafuta, kutoa na kupokea habari.
		• Haki ya mtu kutoingiliwa mawasiliano yake.
		• Haki ya mtu kupewa taarifa wakati wowote.
8	**Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo** ***(Ibara ya 19)***	• Haki ya uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini.
		• Haki ya uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.
		• Haki ya uhuru wa kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini kwa hiari.
9	**Uhuru wa mtu kushirikiana na wengine** ***(Ibara ya 20)***	• Haki ya mtu kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine.
		• Haki ya kutoa mawazo hadharani
		• Haki ya kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.
		• Haki ya mtu kutolazimishwa kujiunga na chama chochote au shirika lolote.

10	**Uhuru wa kushiriki shughuli za umma** ***(Ibara ya 21)***	• Haki ya uhuru wa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi.
		• Haki ya kupiga kura na kupigiwa kura
		• Haki ya uhuru wa mtu wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa.
11	**Haki ya kufanya kazi** ***(Ibara ya 22)***	• Kila mtu ana haki ya kufanya kazi
		• Haki sawa, fursa sawa na kwa masharti ya usawa katika kushika nafasi yoyote ya kazi na shughuli yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi.
12	**Haki ya kupata ujira wa haki** ***(Ibara ya 23)***	• Kila mtu ana Haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake.
		• Haki ya malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi anayoifanya mtu.
		• Stahili ya kupata malipo ya haki
13	**Haki ya kumiliki mali** ***(Ibara ya 24)***	• Kila mtu ana haki ya kumiliki mali
		• Kila mtu ana haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo
		• Haki ya mtu kutonyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengineyo bila ya idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili.

4.3 Uhusiano kati ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora.

Utawala bora na haki za binadamu ni mambo yanayokwenda kwa pamoja. Hii ni kutokana na ukweli kamba ukiukwaji wa misingi ya utawala bora unasababisha uvunjaji wa haki za binadamu; na uzingatiaji wa misingi ya utawala bora unasaidia ulinzi na hifadhi ya haki za binadamu. Jedwali lifuatalo linaonesha jinsi misingi ya utawala bora inavyojitokeza katika haki mbalimbali za binadamu:

MISINGI YA UTAWALA BORA	**Haki za Binadamu kwa mujibu wa *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ya Mwaka 1977**
Ushirikishwaji	• Uhuru kuwa na maoni na kueleza fikra zake (Ibara ya 18). • Uhuru wa mtu kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine (Ibara ya 20). • Haki ya raia kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi (Ibara ya 21).
Maridhiano	• Haki na uhuru wa raia wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa. (Ibara ya 21).
Usawa	• Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa. (Ibara ya 12). • Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria (Ibara ya 13). • Haki ya mtu kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake (Ibara ya 13). • Marufuku kwa sheria na mamlaka yoyote kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake (Ibara ya 13).

Utawala wa Sheria	• Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria (Ibara ya 13). • Haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu yatalindwa na kuamuliwa na Mahakama na vyombo vinginevyo vya Mamlaka ya Nchi vilivyowekwa na Sheria au kwa mujibu wa sheria (Ibara ya 13). • Haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu, na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika (Ibara ya 13). • Marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengineyo bila ya idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili (Ibara ya 24).
Uwazi	• Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii (Ibara ya 18).

SURA YA 5

5.0 MISINGI YA UTOAJI WA HAKI

Uzingatiaji wa utawala bora hauhusu tu mhimili wa serikali, bali pia unahusu vyombo vya kutoa haki. Vyombo hivyo ni mahakama, mabaraza yenye asili ya mahakama, kamati za nidhamu na vyombo vingine vinayofanya kazi zenye asili ya kimahakama.

Hivyo, ili kuzingatia utawala bora katika utoaji wa haki, Ibara ya 107A ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ya mwaka 1977, pamoja na sheria mbalimbali, imeweka misingi ambayo vyombo vya kutoa haki vinatakiwa viifuate. Misingi hiyo ni:

- Kuzingatia Katiba na sheria za nchi;
- Kutenda haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi;

- Kutocheleweshа haki bila sababu ya msingi;
- Kutoa fidia stahiki kwa watu wanaoathirika kutokana na makosa ya watu wengine;
- Kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro;
- Kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka; na
- Kuzingatia kanuni za haki ya asili (natural justice).

5.1 Kanuni za Haki ya Asili

Kanuni za Haki ya Asili ni kanuni zinazoongoza kufanya maamuzi ya utoaji wa haki yaliyo ya haki na kwa kufuata utaratibu ulio wa haki. Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi na mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtoa maamuzi ana wajibu wa kufuata kanuni za haki ya asili. Kanuni hizo ni:

- Haki ya Kusikilizwa
- Wajibu wa kutopendelea
- Wajibu wa kutoa sababu za uamuzi

Vyanzo vya kanuni za haki ya asili ni Katiba, sheria mbalimbali za nchi na maamuzi mbalimbali ya mahakama. Ufafanuzi wa kanuni hizo ni kama ifuatavyo:

5.1.1 Haki ya Kusikilizwa

Haki ya kusikilizwa inamaanisha fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na kwa haki. Haki hii inajumuisha kupewa taarifa ya kutosha na ya mapema ya kesi ili kupata muda wa kuandaa majibu ya kesi dhidi yake, kupewa nafasi ya kutoa ushahidi wake kwa ukamilifu (ikiwa ni pamoja na kuita mashahidi), kupewa fursa ya kuwauliza maswali washitaki wake na kupewa fursa ya kuwakilishwa, kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 13 (6) (a) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

5.1.2 Wajibu wa Kutopendelea

Kanuni hii inatamka kuwa, mtu hatakiwi kuwa muamuzi katika kesi yake mwenyewe; na inatokana na msingi kuwa mtoa maamuzi hatakiwi kuwa na upendeleo na asihisiwe kuwa na upendeleo.

Upendeleo unaweza kusababishwa na maslahi binafsi ya mtoa maamuzi, iwe moja kwa moja au vinginevyo.

5.1.3 Wajibu wa Kutoa Sababu za Uamuzi

Mtoa maamuzi ana wajibu wa kutoa sababu za uamuzi wake. Hii ni kwa sababu kila upande katika mgogoro una haki ya kujulishwa sababu za uamuzi uliofikiwa na chombo cha kutoa haki. Uamuzi wa chombo cha kutoa haki unatakiwa uhalalishwe na sababu za kina na ushahidi. Sababu za uamuzi zinausaidia kila upande kujua ni kwanini umeshinda au umeshindwa. Sababu za uamuzi zinaimarisha uwazi katika utoaji wa haki.

HITIMISHO

Ndugu msomaji, bila shaka Kijitabu hiki kimekupatia maarifa ya msingi na muhimu kuhusu utawala bora. Kwa kukisoma Kijitabu hiki, bila shaka umebaini kuwa utawala bora ni nyenzo muhimu sana ya kufanikisha ajenda kuu za nchi yetu na dunia ambazo ni amani, maendeleo endelevu na ustawi wa mwanadamu na jamii kwa ujumla.

Kwa kuwa sasa umejifunza kuhusu utawala bora, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na Policy Forum zinatarajia kuwa kwa nafasi yako utakuwa mdau muhimu wa kujenga jamii ambayo misingi ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu, utu na ustawi wa mwanadamu inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na kuhifadhiwa.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Idara huru ya serikali yenye mamlaka kamili ya kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini.

Tume hii imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 (1) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ya mwaka 1977. Mojawapo ya majukumu yake ni kupokea malalamiko yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukaji wa misingi ya utawala bora.

Policy Forum ni mtandao wa asasi zaidi ya 100 za kiraia za Tanzania zilizoungana pamoja kwa dhamira ya kushawishi mchakato wa uundwaji sera ili kupunguza umaskini,kuleta usawa na demokrasia wakijikita zaidi katika uwajibikaji wa serikali kwa matumizi ya fedha za umma.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2135747/8, 2137125
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

policy forum

Kitalu 14, Barabara ya Sembeti,
Kandoni mwa Barabara ya Bagamoyo
ya zamani, Mikocheni B,
S.L.P 38486, Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2780200/782317434
Tovuti: www.policyforum.or.tz